

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
(VETA)



MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 08 mwezi 04 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA DSM, S.L.P. 40274,
DAR-ES-SALAAM ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

MICHAEL S. MBONAGA S.L.P. _____, PANGANI
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya
PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya PANGANI;

KWA KUWA Mwajiri anefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya
KUWEKA SAKAFU; (TILES) JENGO LA NYUMBA
YA MKEU WA CHUO

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinavyoonyesha namna kazi
itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 700,000, Fundi atafanya kazi ya KUWEKA TILES kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu. Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;
- Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;
- Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundi;
- Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi;na
- Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundi.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI


- Fundi atakabidhiwa eneo la kazi tarehe 08 mwezi 04 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.
- Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.
- Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -


wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi (arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA DSM

Jina: Kassim Guma Amir Saini: 


Wadhifa: Shes Tarehe: 08/04/2022

Mbele ya (Shahidi)


Jina: Fanda R. Allate Saini: 

Wadhifa: Mhandisi wa Mnd Tarehe: 08/09/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: MICHAEL S WBOVAGA Mbele ya Saini: 
Wadhifa: FUNDI Tarehe: 8/4/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: FADALI A. MIAODIKA Saini: 

Wadhifa: FUNDI MSHAWITI Tarehe: 8/04/2022